TOLEO NAMBA 12

OKTOBA - DISEMBA, 2021

Jarida la

# KILIMO ENDELEVU





## HABARI ZA NDANI


- Zaidi ya wananchi 5000 wapatiwa hati za hakimiliki za kimila Wilayani Mufindi…..uk 2
- Profesa Mkenda: Uzalishaji wa mazao ya chakula Kitaifa waongezeka…..uk 3
- Wanawake 515 wapatiwa hati za hakimiliki za kimila Kijiji cha Nundwe…..uk 5


*MAWASILIANO*

**OFISI YA URATIBU**
**PELUM TANZANIA,**
**S.L.P 390, MOROGORO TANZANIA**

*TOVUTI:* www.pelumtanzania.org

*BARUA PEPE:* Info@pelumtanzania.org

PELUM Tanzania

# Zaidi ya wananchi 5000 wapatiwa hati za hakimiliki za kimila Wilayani Mufindi

Shirika la PELUM Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi wamefanikiwa kutoa jumla ya hati za hakimiliki za kimila zipatazo 8,978 kwa wananchi toka vijiji 16 Wilayani humo, ambapo jumla ya wanufaika kufikia 18,000.

Hati hizi zilizotolewa kwa vipindi vitatu tangu mwaka 2016 hadi 2021 zimewezesha Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kunufaika na urasimishaji wa ardhi vijijini kwa kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji 15 ikiwemo kuipima kwa ajili ya kuandaa na kutoa hati za hakimiliki za kimila na taasisi inazozihudumia.

Wananchi wanaopata hati za hakimiliki za kimila wananufaika kwa kuwa na uhakika wa milki ya ardhi yao, pia wanaweza kuzitumia hati hizo kuomba na kupata mikopo ili kujiongezea mitaji kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ambapo tayari baadhi ya wananchi wametumia hati zao kupata mikopo katika taasisi za fedha. "Benki zetu zilizopo Wilaya ya Mufindi zinapokea hati za hakimiliki za kimila kama dhamana kwa ajili ya mikopo na huduma za kifedha", Leonard Jaka Jaka Afisa Ardhi Mtaule wa Halmshauri ya Wilaya ya Mufindi.

Baadhi ya wanufaika wa hati hizo toka Kijiji cha Kipanga ni Bw. Chongo Mng'wang'ule aliyefanikiwa kupima na mke wake Lili Vanyika hivyo kupata hati ya pamoja. Mng'wang'ule anasema kuwa baada ya kupata mafunzo ya haki za ardhi aliona hakuna haja ya kuendelea kuziishi mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke kwa kuona hana haki kumiliki ardhi.

Hivyo aliamua kupima eneo walilonunua na mkewe akishirikisha familia za pande zote mbili ili hata ikitokea amefariki mke wake na watoto wasinyanyasisike. . "Nimeishi maisha ya kugombania ardhi na ndugu zangu wa tumbo moja pia nimeona jinsi wanawake wanavyodhulumiwa ardhi baada ya wenza wao kufariki. Nilichokifanya ni kuwashirikisha ndugu zangu pamoja na wa mke wangu upimaji wa eneo letu la shamba ili wajue mapema kuwa eneo hili lina umiliki wa pamoja na mwenzangu ili asijekusumbiliwa baadae pamoja na watoto wetu" alifafanua Mng'wang'ule.

Naye Esta Mgungile aliyefanikiwa kupima maeneo matatu (Nyumba na mashamba mawili) amebainisha kuwa baada ya kuona kuna migogoro ya mara kwa mara baina ya watoto wa mke mkubwa na mdogo kuhusiana na umiliki wa maeneo, aliona njia sahihi ya kuepukana na migogoro hiyo ya ardhi ya kifamilia ni kuamua kupima maeneo yake ili yawe kwenye usalama zaidi huku akiweka watoto wake kuwa wanufaika wa maeneo hayo ili nao wasije kusumbuliwa na ndugu.

Habakuki Nyamba ambaye amekuwa akipitia adha ya mgogoro wa mipaka kwa kipindi kirefu baina yake na majirani zake na hasa msimu wa kilimo unapoanza amesema upatikanaji wa hati hiyo ni kiambatanisho sahihi kitakachomfanya kwa sasa aishi vizuri na majirani zake kwani wakati wa upimaji kila aliye karibu na shamba lake aliitwa kuthibitisha mipaka yao kwa makubaliano.

"Kwa sasa sitosumbua tena kamati ya maamuzi kusuluhisha mgogoro wa mpaka, nitalima mazao yangu ya chakula nyakati zote pasipo kugombana na majirani zangu. Lakini pia hati hii itanisaidia kuweka dhamana kwenye mabenki kwani kwa sasa nina mpango wa kuiendeleza ardhi yangu kwa kulima pia mazao ya muda mrefu ikiwemo miti" alielezea Nyamba.

***Inaendelea ukurasa wa nne***



***Bw. Chongo Mng'wang'ule na mke wake Bi. Lili Vanyika wakipokea hati ya eneo lao toka kwa* Kamishina wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Iringa Bw. Wenceslaus Mtui**

# Profesa Mkenda: Uzalishaji wa mazao ya chakula Kitaifa waongezeka

Waziri wa Kilimo Profesa Adolf Mkenda (Mb) amesema uzalishaji wa mazao ya chakula Kitaifa na kimkoa katika msimu wa 2020/2021 na upatikanaji wake umefikia tani 18,425,250 kwa mlinganisho wa nafaka ambapo nafaka ni tani10,869,596 na yasiyo nafaka ni tani 7,327,137. Ikilinganishwa na msimu wa 2019/2020 uzalishaji umeongezeka kwa tani 1,903,096 sawa na asilimia 10.5.

"Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/2022 nchini ni tani 14,796,751 ikilinganishwa na uzalishaji (2020/2021), nchi inatarajiwa kuwa na ziada ya tani 3,628,499 za chakula ambapo tani 1,222,103 ni za mazao ya nafaka na tani 2,406,396 ni za mazao yasiyo nafaka. Kiwango hiki cha uzalishaji kitaiwezesha nchi kujitosheleza mahitaji yake ya chakula kwa uwiano wa utoshelevu wa asilimia 125." alisema Profesa Mkenda.

Hayo ameyasema wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya chakula duniani yaliyofanyika viwanja vya shule ya msingi Mandela, Pasua Moshi- Kilimanjaro na kubeba kauli mbiu isemayo ***'Zingatia uzalishaji na mazingira endelevu kwa lishe na maisha bora'***.

Mkenda alibainisha malengo ya maadhimisho hayo na kusema kuwa "Yanakumbusha wajibu wa kila mmoja wetu katika kuzalisha, kuhifadhi, kutunza mazingira na kutumia chakula bora ili kuwa na uhakika wa chakula katika ngazi ya kaya hadi taifa."

PELUM Tanzania kama Mtandao unaofanya kazi na mashirika wanachama Tanzania bara kwa lengo la kuendeleza na kusimamia matumizi ya kilimo cha kiikolojia katika kuboresha maisha ya wakulima wadogo, kuchaguliwa kuwa sehemu ya kamati ya maandalizi wa maadhimisho. Vilevile PELUM Tanzania ilishiriki katika maadhimisho ambapo waliitumia fursa hiyo kufanya maonyesho ya mbegu za asili pamoja na kupika chakula cha asili.

PELUM Tanzania ilipeleka wakulima 10 toka mashirika wanachama ya SMECAO, MIFIPRO, SAIPRO, DMK na Isalnd of Peace ambapo walishiriki kufanya maonyesho ya mbegu za asili na chakula cha asili. Vile vile, PELUM Tanzania kwa kushirikiana na FAO, SWISAID Tanzania, TABIO, Island of Peace, MVIWAARUSHA, MVIWAKI na Slow Food walifanikisha maonesho na upikwaji wa chakula cha asili ambapo zaidi ya washiriki 300 walikula chakula hicho cha asili.

Maonesho hayo ya mbegu yalitumika pia kama sehemu ya mafunzo kwa wageni waliotembelea mabanda ya wakulima hao wakitaka kufahamu kwa upana zaidi kuhusiana na mbegu za asili ambazo watu wengi wameacha kuzitumia kwa sababu mbalimba ikiwemo kupotea kwa mbegu hizo na wengine kuziona hazina thamani tena.

Lakini pia wapo wageni waliotembelea mabanda hayo kwa lengo la kuomba mbegu ili waweze kuziendeleza kupitia mashamba yao. Moja ya wageni hao ni Mchungaji John Ankway toka kanisa la Angelikani Pasua Kilimanjaro. Anasema yeye alikuwa akilima mahindi ya asili aina ya mehhe na anakumbuka mara ya mwisho kulima ni mwaka 2006 ambapo alilima kwa kuchelewa na hivyo kupoteza mbegu hizo kwani hakuvuna chochote.

Baada ya hapo hakufanikiwa tena kuzipata mbegu hizo hadi alipotembelea mabanda ya wakulima ambao wanatoka mashirika wanachama wa PELUM Tanzania na kuchukua mbegu hizo. Ankway anasema "Nimelima kwa muda mrefu mahindi haya ya asili, shamba la ukubwa wa ekari moja

***Inaendelea ukurasa wa sita***




***Waziri wa Kilimo Profesa Adolf Mkenda (Mb), akihutubia wananchi siku ya kilele cha maadhisho ya siku ya chakula duniani Mkoani Kilimanjaro.***

# Zaidi ya wananchi 5000 wapatiwa hati za hakimiliki za kimila Wilayani Mufindi

***Inatoka ukurasa wa pili***

Mbali na baadhi ya wanufaika wa hati hizo toka Kijiji cha Kipanga kuelezea jinsi hati hizo zitakavyokuwa msaada kwao, lakini bado zipo baadhi ya changamoto zinazobainishwa na viongozi wa Kiserikali Wilayani humo ambazo zinahitaji kuchukuliwa hatua za haraka ikiwemo utoaji wa elimu juu ya sheria za ardhi hasa kwenye vijiji ambavyo havijafanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi na utoaji wa hati za hakimiliki za kimila.

Moja ya changamoto iliyobainishwa na Mkurugenzi wa Halmshauri ya Wilaya ya Mufindi Bi. Zaina Mlawa ni kuhusiana na matumizi mabaya ya mihuri inayomilikiwa na wenyeviti wa vijiji.

"Wapo baadhi ya wenyeviti wa vijiji ambao wamekuwa sehemu ya kuchochea migogoro ya ardhi hasa kwenye vijiji ambavyo havijafanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi na hii ni baada ya kubainika kuwa wanaridhia na kuidhinisha uuzaji wa maeneo kwa mtu zaidi mmoja wakitumia muhuri wa ofisi. Hali ambayo inachochea migogoro ya mara kwa mara ya ardhi baada ya waliouziwa maeneo hayo kugundua wapo zaidi ya mmoja kwenye eneo moja na wote wana vithibitisho halali toka kwa mwenyekiti wa kijiji." alifafanua Bi. Zaina

Mbali na utoaji wa elimu hiyo ya sheria za ardhi kwa viongozi wa vijiji, Bi. Zaina aliongeza na kusema kuwa, kama maeneo hayo yangekuwa yameshapimwa na wananchi kupatiwa hati zao ingekuwa rahisi kwa wananchi wenyewe kumaliza migogoro hii kwa kuwa muhusika wa eneo anakuwa tayari na hati yenye kuonesha umiliki halali.

Naye Kamishina wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Iringa Bw. Wenceslaus Mtui akigawa hati hizo aliwaambia wanakijiji wa Kipanga kuwa "Awali kabla ya kupata hati hizi ardhi yenu ilikuwa inahesabika kama mtaji mfu kwa kuwa kama ungependa kuiendeleza zaidi kwa kukopa fedha benki usingeweza kuonesha eneo lako liwe dhamana bila kuwa na kiambatanisho chenye kuonesha umiliki wako halali, lakini kwa sasa mmefanikiwa kubadili ardhi yenu na kuwa mtaji hai. Hivyo hati hizi ni msaada tosha kwenu kuweza kufanya maendeleo makubwa zaidi kiuwekezaji kwenye ardhi hata kwenye elimu za watoto wenu."



Akizungumza ofisini kwake alipotembelewa na timu ya watumishi wa PELUM Tanzania pamoja na wataalamu wa ardhi toka Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Mkuu wa Wilaya wa Mufindi Mh. Saad Mtambule mbali na kutoa shukrani kwa kazi kubwa ambayo Shirika la PELUM Tanzania imefanya wilayani humo kwa kuwahakikishia wananchi usalama wa ardhi zao baada ya kupima maeneo yao na kuwakabidhi hati za hakimiliki za kimila,lakini pia alitumia wasaa huo kuwashauri wadau wengine wa Asasi zisizo za Kiserikali kuisaidia Serikali katika kurasimisha ardhi ya kijiji kwenye vijiji vilivyobaki Wilayani humo.

"Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ina vijiji 121, hadi sasa ni vijiji 52 tu ndivyo vilivyo rasimishwa, kati ya hivyo, vijiji 15 tumesaidiwa na PELUM Tanzania. Basi niwaombe mashirika yasiyo ya kiserikali kuelekeza nguvu zao katika Wilaya hii ili ikiwezekana vijiji vyote 121 vikamilike kupimwa na hatimaye kukomesha migogoro ya ardhi inayo endelea Wilayani humu". Alisema Mh. Mtambule.

Vijiji vilivyopatiwa hati hizo ni Makungu, Ugesa, Usokami, Isaula, Magunguli, Kipanga, Ilogombe, Kilosa Mufindi, Ihanu, Nandala, Mkonge, Igoda, Udumuka, Ikwega, Ihomasa na Nundwe kupitia miradi ya '***Ushiriki wa wananchi katika kuendeleza sekta ya Kilimo'*** na ***'Uhakika wa ardhi kwa wazalishaji wadogo'*** , na ***'Umiliki wetu usalama wa ardhi yetu'***. Iliyotekelezwa na PELUM Tanzania kwa msaada wa watu wa Marekani na shirika la LANDESA sawia.

# Wanawake 515 wapatiwa hati za hakimiliki za kimila Kijiji cha Nundwe

Shirika la PELUM Tanzania na Landesa Tanzania kwa kushirikiana na Halamshauri ya Wilaya ya Mufindi wamefanikiwa kutoa jumla ya hati za hakimiliki za kimila 1055 kijiji cha Nundwe Wilayani Mufindi, kati hizo hati 515 zimetolewa kwa wanawake.

Hati hizo ambazo zimelenga kuongeza ulinzi kwenye ardhi ya mwanamke zitawasaidia kuepukana na dhana iliyojengeka miongozi mwa jamii kuwa mwanamke hana haki ya kumiliki ardhi jambo ambalo ni kinyume na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kifungu cha tatu cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 zinazompa mwanamke usawa katika umiliki wa ardhi.

“Kila mwanamke kama ilivyo kwa mwanaume, ana haki kisheria kupata, kutumia na kumiliki ardhi, hivyo basi hati hizi zilizotolewa leo naamini zitakuwa msada mkubwa kwa wanawake wa kijiji cha Nundwe kwani mbali na kuzitumia kujiimarisha kiuchumi kwa ajili ya ustawi wa familia zenu lakini pia zitawasaidia kupeukana na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiwaathiri zaidi wanawake”. Alisema Monica Muhoja Mkurugenzi wa Shirika la Landesa Tanzania.

Baadhi ya wanawake waliopata hati hizo wameelezea jinsi gani zitakavyokuwa msaada mkubwa kwao kutokana na changamoto mbalimbali walizopitia kutokana na jamii kuamini kuwa mwanamke hana haki kumiliki ardhi.

Bi. Ziada Mdemu mjane wa watoto sita toka kitongoji cha Mbugani, Kijiji cha Nundwe anasema kabla ya mume wake kufariki mwaka 2015 walifanikiwa kuwa na eneo la ekari sita ambapo ekari mbili walirithishwa na wazazi wa mume wake huku ekari nne wakishirikiana kununua na mume wake.

Maeneo hayo waliyatumia kulima mazao ya miti aina na paini, parachichi pamoja na kulima mazao ya chakula kama vile mahindi, maharage, njegere na viazi vitamu. Bi. Ziada anasema baada ya mume wake kufariki, ndugu wa mume walianza kumnyanyasa ikiwemo kutaka kuchuka ardhi yao yote pamoja na mazao ya muda mrefu waliyokuwa wamepanda.

Hali hii ilimfanya Ziada ajione anapoteza haki zake za msingi pamoja na watoto wake. Pamoja na kufuata sheria kwa kupeleka malalamiko yake kwenye kamati ya maamuzi na Baraza la ardhi la kijiji bado migogoro haikuisha.

Anasema aliposikia kijiji chao kinafanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi, aliwashirikisha watoto wake na kuona ipo haja ya kushiriki zoezi la upimaji wa maeneo yao ili kuweza kuepukana na migogoro ya kifamilia. “Niliona upimaji wa eneo hili ni njia salama na niliamua kuwaweka watoto wangu kama sehemu ya wanufaika ili hata ikitokea nimefariki wasisumbuliwe na ndugu, kwani kwa sasa hata serikali ya kijiji inatambua umiliki halali wa kisheria wa eneo hili hivyo yeyote atakayetusumbua tutamwambia atuonyeshe uhalali wake wa kumiliki ardhi hiyo” amesema Bi. Ziada.

***Inaendelea ukurasa wa saba***



***Bi. Felista Kalinga mjane wa watoto sita toka Kijiji cha Nundwe, akipokea hatimiliki ya eneo lake toka kwa Mkuu wa Wilaya wa Mufindi Mh. Saad Mtambule***

# Profesa Mkenda: Uzalishaji wa mazao ya chakula Kitaifa waongezeka

***Inatoka ukurasa wa tatu***

Ankway anasema "Nimelima kwa muda mrefu mahindi haya ya asili, shamba la ukubwa wa ekari moja nilikuwa nikipata magunia 18-20 na sikuwa nikitumia mbolea wala madawa ya viwandani kama njia ya kuongeza uzalishaji. Maonyesho haya yamenijereshea furaha yangu kwani mbali na kuwa nitapanda mahindi haya kwa msimu wa 2021/2022 bado nitakuwa na uhakika wa mbegu kwa miaka mingine mbele kwani mkulima yeyote anauwezo wa kurudia kupanda mbegu hizo shambani kwake tofauti na mbegu za kisasa ambazo inampasa mkulima kila mwaka anunue mbegu nyingine."



***Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mh. Steven Kagaigai akipokea zawadi ya boga toka kwa mmoja wa wakulima wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya siku ya chakula duniani. Mh. Kagaigai ni mmoja kati ya viongozi waliochukua mbegu za asili toka kwa wakulima kwa ajili ya kilimo.***

Maonyesho hayo yaliwawezesha wakulima kubadilishana mbegu aina tisa ikiwemo aina 5 za mahindi (40 kg), aina 34 za maharage (86 kg), alizeti (24 kg) na fiwi (14 kg)



***Mmoja wa wageni waliotembelea mabanda ya wakulima wakati wa maadhimisho ya siku ya chakula duniani yaliyoambatana na maonyesho ya mbegu na chakula cha asili, akijifunza umuhimu wa matumizi ya mbegu za asili toka kwa mkulima wa Shirika la MIFPRO***

Akifungua maadhimisho ya siku ya chakula duniani, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mh. Steven Kagaigai aliwaasa watafiti na masharika yanayotekeleza kilimo cha kiikolojia ikiwemo PELUM Tanzania kuhakikisha wanaendeleza mbegu za asili ambazo zinampa mkulima uhuru mkubwa wa kuzitumia zaidi ya mara moja.

Lakini pia aliyaasa mashirika hayo kuendelea kupaza sauti hasa wakati wa maboresho ya sera mbalimbali kuhusu mbegu kwa kuwa wao ndio wenye uelewa zaidi kuhusiana na uhalisia wa mbegu za asili ambazo zinamuondolea mkulima utumwa wa kununua mbegu kila msimu wa kilimo.

# Wanawake 515 wapatiwa hati za hakimiliki za kimila Kijiji cha Nundwe

*Inatoka ukurasa wa tano*

Si Ziada peke yake anayekumbana na changamoto hizo za migororo ya ardhi ya kifamilia bali pia Felista Kalinga mjane wa watoto sita. Yeye anasema kifo cha mume wake kilichotokea mwaka 2009 kilimfanya aondolewe na ndugu wa marehemu mume wake kwenye nyumba waliyojenga kwenye eneo walilopewa na baba mkwe wake.

Felista anasema tangu kufariki kwa mume wake ofisi ya Mtendaji wa kijiji imekuwa kama nyumbani kwake kutokana na vitisho alivyokuwa akipewa na shemeji zake. Anasema kuitwa kwa ndugu wakubwa baba mkwe wake waje kuthibitisha uhalali wake wa kukaa kwenye eneo hilo ilisaidia kupunguza kidogo mgogoro baina yake na ndugu wa marehemu mume wake. Kwa sasa Felsta anafuraha baada ya kupokea hatimiliki ya kimila ya eneo lake lililokuwa na migogoro.

"Naishukuru sana Serikali ya kijiji cha Nundwe kwani walivyosikia kuna wadau wamejitokeza kupima maeneo yetu walinishirikisha ili nami nipimiwe eneo langu ili niweze kuondokana na mgogoro wa kifamilia kwenye eneo langu uliodumu miaka mingi." Amesema Bi. Felista

Naye Oliva Msungu kijana wa miaka 30 na mama wa mtoto mmoja anasema baada ya kuolewa tu alikutana na vitisho toka kwa ndugu wa mume wake wakisema mbele yake ***'hakuna mtoto wa kike anayeruhusiwa kumiliki ardhi, siku zote ardhi ni ya mtoto wa kiume na ndio mwenye mamlaka nayo kuifanyia lolote tena pasipo hata kumshirikisha mke wake'.***

Anasema maneno hayo yalikuwa yakimuumiza moyoni na hasa anapokumbuka kanunua eneo na mume wake robo ekari ambalo wamejenga nyumba wanayoishi. Lakini akigeuka nyumba ya pili alikuwa akiona mama mjane anavyonyanyaswa na ndugu wa marehemu mume wake kumtaka aachie mali zote walizochuma na mume wake.

Hofu hii aliyoibeba kwa muda mrefu kuhusiana na umiliki wa ardhi kwa mwanamke ilifika kikomo baada ya kupata elimu juu ya sheria za haki za ardhi Iliyotolewa na Shirika la PELUM Tanzania kwa kushirikiana na wataalamu toka Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi wakati wakijiandaa kufanya upimaji wa vipande vya ardhi vya wananchi kijiji cha Nundwe.

"Wakati nimehudhuria mafunzo ya sheria za ardhi niliskia wakisema kuwa mwanamke ana haki sawa na mwanaume kupata, kutumia na kumiliki ardhi lakini pia mume na mke wanaweza kumiliki eneo kwa pamoja."

Kipengele cha umiliki ardhi wa pamoja kilimpa nguvu na kwenda kumshirikisha mume wake juu ya kupata hati ya pamoja ili waweze kumiliki eneo lao kihalali. Baada ya kumshirikisha mume wake aitwaye Fredrick Lunyungu adhima ya kumiliki eneo lao kwa pamoja ikiwemo faida zake, mumewe hakusita kukubaliana naye. Kwa sasa wamefanikiwa kupata hatimiliki ya kimila ya pamoja ambayo inawahakikishia usalama wa milki ya ardhi yao.

Akihitimisha zoezi hilo la ugawaji wa hati za hakimiliki za ardhi, Mkuu wa Wilaya wa Mufindi Mh. Saad Mtambule aliwasisistiza wananchi wa kijijiji cha Nundwe na hasa waliopima mashamba kuhamasika kupanda mazao ya muda mrefu kwenye mashamba hayo na hasa miti pamoja na miche ya matunda aina ya maparachichi kwa kuwa sasa maeneo yao yako salama na hakuna mtu atakayewavamia na kuharibu mali zao kwa kisingizo kuwa lilikuwa eneo lake.

Lakini pia alitumia fursa hiyo kuwahamasisha wananchi ambao wamekuwa waoga kupima maeneo yao kwa dhana kuwa serikali ina nia ovu ya kuyachukua, waige mfano wa wenzao ambao kwa sasa wana hati zao mikononi na ardhi zao tayari zimepanda thamani baada ya kupimiwa na serikali haijayachukua hayo mashamba.

